REVIVAL NEWS
From **Revival Ministries Australia**
P.O. Box 2718 BC TOOWOOMBA Q4350 Australia
Phone: 61-7-46130633; e-mail: rma@revivalministries.org.au
Website: www.revivalministries.org.au

****MACHI 2021****MACHI 2021****MACHI 2021****

TOBA

Tuko katika wakati wa kupitia "***kuburudika kidogo"* Ezra 9:8.** Nakala ya King James inasema ***"ufufio kidogo".*** Katika muktadha huu tumebarikiwa kuwa wenyeji wa mkusanyiko wa maombi katika jiji zima ambao umekuwa ukiwavutia watakatifu kutoka kwa ushawishi mbalimbali wa "kanisa" kuja pamoja na kuomba. Hii imekuwa ya ajabu na Mungu amekuwa akitutembelea katika njia tofauti na kuleta matokeo tofauti. Katika mkutano mmoja wa maombi hivi majuzi alikuwa akitunenea kuhusu hitaji la kuombea watu na kushiriki na watu hitaji la ***kutubu.*** Ni ujumbe wa wakati kwa sisi kutia nguvu msingu huu wa ***kuzitubia kazi zisizo na uhai* (Wabrania 6:1)** kuchunguza eneo la ***toba*** kwa njia mpya.

PICHA MBILI ZA TOBA

1. Kuchimbua udongo wa mashamba

Mungu anaongea na **Hosea** kwa sisi ***"uchimbueni udongo wa mashamba yenu yasiyolimwa, kwa maana wakati umewadia wa kumtafuta Yahweh, hata atakapokuja na kuwanyeshea haki"* 10:12.** *Udongo usiolimwa* ni udongo ambao umeachwa bila kulimwa, umeachwa pekee. Hii ni kipengele muhimu katika ukulima kuacha ardhi kupumzika. Hata hivyo, ardhi uapoachwa bila kulimwa, chochote hukua, na ardhi unaweza kuwa ngumu. Inahitaji kuvunjwa ili iwe ya faida tena kwa kile mkulima anataka kukuza. Mungu kimsingi hatupi funzo katika ukulima. Hii ni picha ya umuhimu wa ***toba*** kufanya kazi ndani yetu kuvunja ardhi ya mioyo yetu isiolimwa, kuwa tayari ku "***jipandieni katika haki, vuneni kwa fadhili"* Hosea 10:12.**

Kutayarisha mioyo yetu kwa mvua yake

Kuna sehemu nyingi katika mioyo yetu ambayo yameachwa bila kulimwa. Kunaweza kuwa na sehemu ambazo tuna tabia zetu wenyewe, shauku na hakujakuwa sana na Mungu akihusika katika hiyo sehemu ya maisha yetu. Ni wakati wa ***kuchimbua udongo usiolimwa.*** Ni wakati wa kutubu na kubadilika katika sehemu ambazo tumejiwekea na kukubalia Bwana Yesu katika sehemu hizo. Ni wakatiwa kusikia sauti ya Mungu katika kila sehemu katika mioyo yetu, bila kushikilia nyuma sehemu zingine zisizo shikamana katika maisha yetu kwa sisi wenyewe ***"kwa kuwa ni wakati wa kumtafuta Yahweh"*** na anajitayarisha ***"kuja na kutunyeshea haki". Toba*** inaonekana katika msitari huu kama ***kuchimbua ardhi isiolimwa.*** Hii inaweza kuwa ngumu kufanya, kulingana na jinsi udongo wa mioyo yetu umekuwa mgumu. Lakini ni muhimu kutoa mavuno ambayo Mungu anatafuta!

2. Toa mawe nje

Mungu alinena kupitia kwa **Isaya** akisema, ***"Piteni, piteni, katika malango! Itengenezeni njia ya watu; tutieni, tutieni barabara! Toeni mawe yake; Twekeni bendera kwa ajili ya kabila za watu"*** **62:10.** Mungu anatuita ***kupita malango.*** Yesu hatutaki nje bali kuingia ndani ya mji wake na makusudi yake! Anatuita ***kutengeneza njia ya watu!*** Yesu anataka tutangulize na kuweka mfano wa njia kwa watu kufuata. Ili tuweze kusema, ***"Mnifuate mimi kama mimi ninavyomfuata Kristo"*** **(1Kor.11:1).** Anatuita ***"kutia barabara!*** Yesu anataka tutie ***"barabara ya utakatifu"*** **(Is.35:8),** kuonyesha maisha ambayo imewekwa wakfu kwa makusudi yake. Ili kufanya hii, ni lazima ***"tutoe mawe nje!"*** Mawe hutukwaza. Mawe ya dini ya mtu, mila, imani za kidhehebu na njia, lazima ***zitolewe kwa njia!*** Hii ni ***toba kutoka kwa kazi zilizokufa za kidini!***

Toa kikwazo katika njia

Isaya anasema mahali pengine, ***"Tutieni! Tutieni!*** **Itengenezeni** ***njia, kiondoeni kila kikwazacho katika njia ya watu wa Mungu"*** **57:14.** Mawe haya ni vikwazo. Yanawafanya waumini kujikwaa na kutopokea yote ambayo anayo kwao. Yanazuia waumini kutopitia ukamilifu wa Mungu! Mawe haya ni mafundisho ya kidini ambayo yanafanya watu kutoamini yale ambayo yameandikwa wazi katika neno la Mungu. Yanainua mila za binadamu na elimu ya dini juu ya mamlaka ya Maandiko yenyewe, kusema kwamba hakuna manabii leo, hakuna miujiza tena, hakuna dhihirisho la vipawa tena**,** hakuna kuongea kwa ndimi tena na kufanya watu wa Mungu kujikwaza.

Toa kikwazo katika njia! Tubu na ***"Hasha! Mungu aonekane kuwa amini na kila mtu mwongo!"*** **(Warumi 3:4).** ***"Na yeyote <u>atakayewakosesha</u> mojawapo wa wadogo hawa waniaminio, afadhali afungiwe jiwe la kusagia shingini mwake mwake, na kutupwa baharini"*** **Marko 9:42.** Huo ndio mtazamo wa kumaanisha wa Yesu kuhusu vikwazo hivi! ***Zitoeni kwa njia!***

Ufufio hujia wanyenyekevu na waliotubu

Tunahitaji kurudi kwa ***toba kutoka kwa kazi zilizokufa.*** Kubadilisha nia yetu na kunyenyekea. Mungu anaahidi, ***"Maana yeye aliye juu, aliyetukuka, akaaye milele; ambaye jina lake ni Mtakatifu; asema hivi; Nakaa mimi mahali palipoinuka, palipo patakatifu; tena pamoja na yeye aliye na roho iliyotubu na kunyenyekea, ili kuzifufua roho za wanyenyekevu, na kuifufua mioyo yao waliotubu"*** **Isaya 57:15.** Ufufio hujia wale walionyenyekea na wametubu. Wale ambao ***"wanatetemeka wanaposikia neno langu"*** **(Is.66:2).**

TOBA NA INJILI

Neno ***toba*** katika Agano Jipya ni neno la kigiriki *metanoeo* na linamaanisha *kufikiria kitofauti au baadaye,* yaani, *kufikiria tena* (Strong's Gk.#33). Linaweza pia kumaanisha: kuona *baadaye* kwa vile sehemu ya kwanza ya neno *meta* linamaanisha: *baada, kuashiria 'mabadiliko'* na sehemu ya pili *noeo* linamaanisha *kuona, kutoka 'nous' ambalo ni 'nia, kiti cha fikra mema'.* Hili ni neno la ndani. ***Kutubu*** linamaanisha kurudia tena na kufikiria juu ya fikra zako na tabia kwa njia ya kufanya uamuzi wa kufikiria tofauti na kubadilika! Ni kufikiria juu ya kitu baadaye na kufanya uamuzi kwa ujuzi kubadili njia zako kutoka wakati huo kwenda mbele. Tunahitaji kukubalia toba kufanyika ndani ya maisha yetu na maisha ya wengine!

Mahali mwafaka ya toba katika injili

Yohana Mbatizaji alihubiri toba kama njia muhimu ya kuitikia ufalme wa mbinguni kuja kwetu, ***"Tubuni, kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia"*** **Mathayo 3:2.** Yesu alihubiri ujumbe uo huo katika **Mathayo 4:17.** Ili kuingia na kupitia ufalme wa mbinguni inahitaji sisi *kufikiria tofauti na kuangalia maisha na mwenendo wetu.* Yesu alipowatuma wale kumi na wawili kwa kazi kimisionari inasema, ***"Wakatoka, wakahubiri kwamba watubu. Wakatoa pepo wengi, wakapaka mafuta watu wengi waliokuwa wagonjwa, wakawaponya"*** **Marko 6:12-13.** Wale kumi na wawili walihubiri nini? ***Kwamba watu watubu!*** Hiki ndicho kiitikio kinachofaa kwa ujumbe wa ufalme wa Mungu. Matokeo ni kwamba wengi walikombolewa kutokana na pepo na kupakwa na kuponywa.

Toba na Utume

Maneno ya mwisho ya Yesu yaliyonakiliwa katika injili ya **Luka** yanahusisha amri ya mwisho ya Yesu na maagizo na mara nyingi tunaita "Tume". Yesu alisema, ***"Ndivyo ilivyoandikwa, kwamba Kristo atateswa na kufufuka siku ya tatu, na kwamba mataifa yote watahubiriwa kwa jina lake habari ya toba na ondoleo la dhambi, kuanza tangu Yerusalemu"*** **Luka 24:46-47.** Ujumbe rahisi wa injili ni kuhubiri Kristo kuwa yeye ni, na yale aliyoyafanya kulingana na Maandiko na kisha kuhubiri kwamba watu wanafaa ***kutubu*** kuitikia ujumbe na kupokea ***ondoleo la dhambi katika jina lake.***

Petro alitii utume

Petro alifanya hii kwa utiifu siku ya pendekote kwa kuhubiri Kristo kwa nguvu, kuonyesha kwamba ***"Mungu amemfanya Yesu huyo mliyemsulubisha kuwa Bwana na Kristo"*** **Matendo 2:36.** Watu walitaka kujua wafanye nini na huu ufunuo wa ajabu **(Matendo 2:37).** Petro aliwaambia, ***"Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu"*** **Matendo 2:38.** Kiitikio cha injili sio "kuja vile ulivyo" au "kuinua mkono". Kiitikio ni ***kutubu na kubatizwa.*** Badilisha nia yako, fikiria tena juu ya imani zako na njia zako, fikiria tofauti kuhusu yale ambayo unafikiri Yesu ni, na yale ambayo amefanya, na uamue kuweka tumaini lako kwake, ubatizwe katika jina lake na dhambi zako ziondolewe!

Mungu hujalia toba

Toba ni kipawa kutoka kwa Mungu. Ni kipawa cha ajabu. Ni uwezo wa kubadilika. Petro alisema, ***"Mtu huyu Mungu amemtukuza kwa mkono wake wa kuume, awe Mwokozi, awape Waisraeli toba namsamaha wa dhambi"*** **Matendo 5:31.** Mungu hutupa toba ili dhambi zetu ziweze kusamehewa. Paulo alimwambia Timotheo kwamba kama watumishi wa Bwana hatupaswi ***"kuwa mgomvi; bali kuwa mwanana kwa watu wote, awezaye kufundisha, mvumilivu; akiwaonya kwa upole wao washindanao naye, ili kama ikiwezekana, Mungu wape kutubu na kuijua kweli"*** **2 Timotheo 2:24-25.** Mwenendo wetu na jinsi tunavyowasilisha ukweli unaweza kuwafungulia wengine mlango kutubu na kuja kujua kweli. Lakini ni Mungu ***anayejalia toba.*** Kwa hivyo wacha tugeukie maombi kwa wale wanaoshindana na injili, ili Mungu awajalie toba na msamaha wa dhambi ***ili waweze kujua kweli!***

Mungu anaamuru watu wote kutubu

Toba sio tu kitu kizuri kufanya. Ni amri. Ni lazima tutubu. ***"Basi, zamani zile za ujinga Mungu alijifanya kama hazioni; bali sasa anawaagiza watu wote wa kila mahali watubu. kwa maana ameweka siku atakayowahukumu walimwengu"*** **Matendo 17:30-31.** Kwa kutazamia

hukumu unaokuja ni juu ya sisi sote kuwa tayari kubadilika, kufikiria tofauti na kuchunguza kwa wema njia zetu. Wayahudi wengine walipofikiri kwamba pengine hukumu kali ilikuja kwa watu fulani kwa sababu walikuwa ***"wenye dhambi zaidi",*** Yesu aliwakumbusha kukaa timamu akisema, ***"lakini msipotubu, ninyi nyote mtaangamia vivyo hivyo"*** **Luka 13:3-5.** Mungu anaamuru sisi sote kutubu!

Toba na imani-misingi ya maisha yetu katika Kristo

Mwandishi kwa **Waebrania** alisema alitaka ***"kuacha kuyanena mafundisho ya kwanza ya Kristo ,… tusiweke msingi tena wa kuzitubia kazi zisizo na uhai, na kuwa na imani kwa Mungu"*** **Waebrania 6:1.**Toba sio kitu unafanya mara moja! Ni fundisho la kimsingi kwa maisha yetu katika Kristo, ***fundisho la kwanza la Kristo.*** Tunaishi katika maisha ya toba sasa, kila wakati tukiwa tayari kubadilisha nia yetu, mtazamo na tabia jinsi tunavyoguzwa na ukweli wa Neno na Roho wa Mungu. Ni muhimu kukaa kando na mtego wa ***kazi zisizo hai.*** Kwa muktadha huu hizi ni kazi zisizo na uhai za kidini; kujaribu kumpendeza Mungu kwa kushika mila fulani, matendo, njia za utumishi na kupitia kwa kushika sheria na mafundisho ya kidini. Ni lazima tutubu kutoka kwa hizi na kugeukia ***imani kwa Mungu.*** Paulo kama mtume alifundisha hii popote alipokwenda, ***nikiwashuhudia Wayahudi na Wayunani wamtubie Mungu, na kumwamini Bwana wetu Yesu Kristo"*** **Matendo 20:21.** Je, unaweka misingi hii na kuziimarisha ndani ya watakatifu kila mahali unapokwenda?

Tunda la Toba

Toba lina kazi ya kuonekana nje. Kuna mabadiliko ya kweli. Waumini wengine wanafikiri toba ni kusikitikia dhambi zako. Nimekutana na watu ambao wanakaa kusikitikia dhambi zao lakini bado hawabadiliki-hawatubu! Paulo aliwasifu wakorintho, "***Sasa nafurahi, sikwa sababu ya ninyi kuhuzunika, bali kwa sababu mlihuzunishwa, hata mkatubu. Maana mlihuzunishwa kwa jinsi ya Mungu…Maana huzuni iliyo kwa jinsi ya Mungu hufanya toba liletalo wokovu lisilo na majuto; bali huzuni ya dunia hufanya mauti"*** **2 Kor.7:9-10.** Haitoshi kusikitika. Kuna hitajika kuwa na uamuzi wa kubadilika. Yohana Mbatizaji alihubiri, ***"Basi zaeni matunda yapasayo toba"*** **Mathayo 3:8.** Mtume Paulo pia alitangaza ***"kwamba watubu na kumwelekea Mungu, wakiyatenda matendo yanayopatana na kutubu kwao"*** **Matendo 26:20.** Kama tutadhibitiwa katika ufufio, huu msingi wa toba lazima ifanye kazi kwa maisha yetu. Toba ni uamuzi wa kubadilika baada ya kutafakari. Kutakuwa na tunda; maisha yaliyobadilika ya imani kwa Mungu!

TOBA KATIKA KANISA

Kuacha upendo wa kwanza

Kanisa katika Efeso lilikuwa na tabia nyingi za kusifika. Walikuwa wanafanya kazi kwa bidi, walionyesha uvumilivu, walikuwa na nguvu kwa ukweli, walichukia uovu, ***"tena ulikuwa na subira na kuvumilia kwa ajili ya jina langu, wala hukuchoka"*** **Ufunuo 2:2-3.** Hawa watakatifu walikuwa wanamfanyia Yesu mengi na hawakuchoka. Walikuwa wamejitolea kweli, lakini Yesu bado alikuwa nashida nao, ***"umeacha upendo wako wa kwanza. Basi wapi ulikoanguka; ukatubu, ukayafanye matendo ya kwanza"*** **Ufunuo 2:4-5.** Neno *'kuacha'* linamaanisha *'walitelekeza'* upendo wao wa kwanza. Walikuwa wanamfanyia Yesu kazi kwa bidi, lakini hawakuwa na uhusiano na Yesu. Walikuwa wamejitolea kwa mambo ya injili, lakini wakaacha kitu cha msingi, kuwa karibu na uhusiano na Yesu.

Tubu na kufanya matendo ya kwanza

Hili ni onyo kwa sisi sote. Yesu aliwaambia ***kutubu na kufanya kazi za kwanza.*** Tumeona *"kazi za kwanza"* kama kurudi kwa kutenda kazi za kwanza za kanisa la kwanza, yaani ***"katika mafundisho ya mitume na ushirika, katika kuumega mkate, na katika maombi*** **Matendo 2:42.** Lakini kumbuka ni kwanza ***tubu*** na kisha ***tenda kazi za kwanza.*** Kutubu huku ni kufikiria tena, ku ***"kumbuka wapi umeanguka".*** Sasa kumbuka wakati ulifanya ***kazi za kwanza*** kutoka kwa kujitoa kwa upendo na uhusiano na Yesu. Kumbuka sio orodha ya kazi za kuweka alama ya sawa "za kufanya" kwa orodha ya kidini. Hizo kazi za kwanza ni matokeo ya uhusiano wetu na Yesu:

- **fundisho la mitume-**kusikiliza neno la Mungu likija kupitia kwa kusoma, kufundisha na kuhubiri Neno lake
- **ushirika-** kusikiliza kile Yesu anasema kupitia watakatifu na kudhihirisha upendo mmoja kwa mwingine
- **kuumega mkate-** kushiriki na kuwa na ufunuo wa Yesu kwa meza yake
- **maombi-** kuongea na Mungu tunapoomba pamoja na kupata uongozi wake

Thawabu ya toba

Ilikuwa kukemewa vikali na Yesu ambapo alionya kwamba ***"nitakuondoa kinara chako katika mahali pake, usipotubu"*** **Ufunuo 2:5b.** Lakini thawabu ya toba na kurudi kwa kazi za kwanza kutokana na upendo kwa Yesu ilikuwa, ***"nitampa kula matunda ya mti wa uzima, ulio katika bustani ya Mungu"*** **2:7.** Toba ni kutoka kwa ***kazi zisizo hai.*** Inaonekana Yesu alikuwa anaashiria kwamba kanisa la Efeso lilikuwa likila kutoka kwa mti mbaya. Walikuwa wameanza kuwa wa kidini katika kujitoa kwao kwa injili na kuanza kula kutoka kwa mti wa kujua mema na baya. Toba ingewarudisha kutumaini, tegemea na kupenda Yesu, kula kutoka kwa ***mti wa uzima*** na kupitia ***paradiso ya Mungu.***

Kuwa na raghba na utubu

Yesu pia alinena na kanisa la Laodekia kuhusu mambo mengi kuhusu mtazamo wao wa juujuu kwa injili na kufikiri mali yao ya kimwili ilimaanisha wamebarikiwa na Mungu, ***"mimi…wala sina haja ya kitu"*** **Ufunuo 3:17a.** Hali yao ya kiroho ilikuwa katili, ***"u mnyonge, na maskini, na kipofu, na uchi"*** **mst. 17b.Yesu** aliwatuliza katika ukosoaji wake mkali, ***"wote niwapendao mimi nawakemea, na kuwarudi; basi uwe na bidi, ukatubu"*** **mst.19.** Kama waumini sote tunakua na sisi, hata kwa pamoja, tunaweza kwenda kando kwa urahisi. Tumsifu Mungu kwamba anatupenda sana hivi kwamba atatukabili na kutukemea tunapohitaji. Kwa sababu tuko katika safari ya kukua lazima tuwe tayari ***kutubu.*** Tunafaa kubeba mtazamo wa kutubu, kuwa tayari kubadilika na kufikiria tena njia zetu na kupokea marekebisho ambayo Bwana Yesu anatuletea. Hii ndiyo njia tu ya kubaki katika ufufio!

Thawabu

Yesu aliambia kanisa lake, ***"Tazama, nasimama mlangoni, nabisha; mtu akiisikia sauti yangu, na kufungua mlango, nitaingia kwake, name nitakula pamoja naye, nayeye pamoja name"*** **Ufunuo 3:20.** Toba ni kudumisha moyo mwepesi, kusikiliza sauti yake kuitika kwa ***kufungua mlango*** wa mioyo yetu kwa Yesu. ***"Leo kama mtaisikia sauti yake, msifanye migumu mioyo yenu"*** **Waebrania 3:15.** Toba ni kuwa tayari kusikiliza sauti ya Roho wa Mungu ndani yetu, akituchochea, kutufundisha na kuturekebisha. Kisha kuwa tayari kufanya maamuzi kulingana na yale tunayosikia. Matokeo yatakuwa, ***"nitampa kuketi pamoja nami***

katika kiti changu cha enzi, kama mimi nilivyoshinda nikaketi pamoja na Baba yangu katika kiti chake cha enzi" **mst.3:21.** Moyo na maisha ya kutubu inastahili! Utaishia kupitia kuketi na Kristo katika ulimwengu wa roho (**Waefeso 2:6).**

Kukaa katika ufufio lazima tukaze msingi wa toba katika masha yetu.
Baki wazi kwa mabadiliko.
Udongo wako usiolimwa uchimbuliwe.
Kubali Bwana Yesu kukukabili, kukukemea
na kurekebisha maisha na mwenendo wako.
Ni wakati wa kumtafuta Yesu hadi atunyeshee haki!